

Simu : +255 (026) 2322703  
Nukushi : +255 (026) 2322704  
Baruapepe: [km@uchukuzi.go.tz](mailto:km@uchukuzi.go.tz)  
Tovuti: <https://www.uchukuzi.go.tz>



Mji wa Serikali Mtumba, 1 Mtaa wa  
Ujenzi,  
S. L. P 638,  
**40470 DODOMA.**

## TAARIFA KWA UMMA

### MKUTANO WA KUPOKEA MAONI YA WADAU KUHUSU MAPENDEKEZO YA MABORESHO YA SHERIA NA BAADHI YA KANUNI ZA MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI (LATRA)

**Dodoma,  
Tarehe 28 Mei, 2024.**

Wizara ya Uchukuzi kwa mujibu wa kifungu cha 45 cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini Sura ya 413 inawaalika wadau wote wa usafiri ardhini kuhudhuria mkutano wa kupokea maoni kuhusu mapendekezo ya maboresho ya Sheria na baadhi ya Kanuni za Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA). Mkutano utafanyika tarehe 5 Juni, 2024 katika Ukumbi wa Mikutano wa Arnaoutougrou uliopo Mnazi mmoja, Dar es Salaam kuanzia saa tatu kamili (3:00) asubuhi.

#### A. SHERIA

- i) Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini Sura ya 413;
- ii) Sheria ya Leseni Sura ya 317;

#### B. KANUNI

- iii) Kanuni za Huduma za Kukodi za Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini Tangazo la Serikali Na. 78 la Mwaka 2020;
- iv) Kanuni za Huduma za Usafiri wa Umma za Leseni Leseni za Usafirishaji Tangazo la Serikali Na. 76 la Mwaka 2020;
- v) Kanuni za Vyombo vya Kubeba Mizigo za Leseni za Usafirishaji Tangazo la Serikali Na 77 la Mwaka 2020;
- vi) Kanuni za Utaratibu wa Kushughulikia Malalamiko za Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini Tangazo la Serikali Na. 26 la Mwaka 2024; na
- vii) Kanuni za Vigezo na Masharti ya Kutoa Huduma zinazodhibitiwa za Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini Tangazo la Serikali Na. 27 la mwaka 2024.

Mapendekezo haya yanapatikana kwenye tovuti ya Mamlaka <https://www.latra.go.tz> sehemu ya Sheria.

**Imetolewa na:**

Prof. Godius Kahyarara

**KATIBU MKUU - UCHUKUZI**